



GRETCHEN WHITMER
GOVERNOR

STATE OF MICHIGAN
OFFICE OF THE GOVERNOR
LANSING

GARLIN GILCHRIST II
LT. GOVERNOR

AMRI YA UTENDAJI

No. 2020-14

Kuahirishwa kwa muda kwa tarehe ya mwisho ya kukomboa mali yaliyochukuliwa kwa kukosa kulipa ushuru wa mali

Kirusi kipya cha Korona (COVID-19) ni ugonjwa unaohusiana na upumuaji na unaweza kusababisha kuugua vibaya au kifo. Ugonjwa huu unaletwa na aina ya kirusi cha Korona ambacho hapo awali hakikuhusiana na binadamu na kinachoambukizwa kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine. Hadi sasa hakuna chanjo iliyoidhinishwa au matibabu ya kuzuia ugonjwa huu.

Tarehe 10 mwezi wa tatu mwaka wa 2020, Idara ya Afya na Huduma za Watu ya Jimbo la Michigan iligundua visa viwili vya kirusi cha COVID-19 katika jimbo Michigan. Siku hiyo hiyo, nilitoa Amri Kuu ya Utendaji 2020-4. Amri hii ilitangaza hali ya dharura katika jimbo lote la Michigan chini ya sehemu ya 1 ya kifungu cha tano cha Katiba ya Michigan ya 1963, Sheria ya Usimamizi wa Dharura, 1976 PA 390, ilivyofanyiwa marekebisho, MCL 30.401-421, na Sheria ya Nguvu za Dharura za Gavana ya 1945, 1945 PA 302, ilivyofanyiwa marekebisho, MCL 10.31-33.

Sheria ya Usimamizi wa Dharura inampa Gavana mamlaka mapana na majukumu “kukabiliana na hatari zinazotisha jimbo hili au watu wa jimbo hili kutokana na janga au jambo la dharura,” ambazo Gavana anaweza kutekeleza kupitia “amri kuu ya utendaji, matangazo, na amri zilizoidhinishwa kisheria.” MCL 30.403(1)-(2). Vile vile, hii Sheria ya Mamlaka ya Dharura ya Gavana ya 1945, imeeleza kwamba, baada ya kutangaza hali ya dharura, “Gavana anaweza kutoa maagizo, sheria na kanuni atakazoziona kuwa za lazima kulinda maisha na mali au kudhibiti hali ya dharura katika sehemu husika.” MCL 10.31(1).

Kufuatana na ugonjwa wa COVID-19, ofisi nyingine za Kaunti zimefungwa au zimepunguza ruhusa ya kuingia kwenye majengo ya Kaunti. Kutokana na hali hii, waweka hazina wengi wa Kaunti wameshindwa kuchakata malipo ya ukombozi au kufanya mipango ya malipo na watu wanaomiliki mali, kama vile nyumba, ili kuzuia mali hayo kuchukuliwa na kampuni zilizotoa mikopo ya kununua mali hiyo.

Ili kupunguza usambazaji wa kirusi cha COVID-19, kulinda afya ya umma na kutoa ulinzi muhimu kwa watu wa jimbo la Michigan walio kwenye hatari mbalimbali, ni jambo la maana na lazima kuahirisha kwa muda sheria na taratibu ili kusongesha mbele tarehe ya mwisho ya kukomboa mali yaliyochukuliwa na kampuni iliyotoa mkopo kwa kusosa kulipa ushuru wa mali hayo.

Kwa kutumia maagizo ya Katiba ya Michigan ya mwaka 1963 na sheria ya Michigan, ninaamuru yafuatayo:

1. Kufuatiliwa kwa sehemu ndogo ya sehemu 78g ya Sheria ya Ushuru wa Jumla wa Mali (GPTA”), 1893 PA 206, ilivyofanyiwa marekebisha, MCL 211.78g(3) umeahirishwa kwa mda. Kufuatana na hii, tarehe ya mwisho ya kukomboa mali yalikabidhiwa mweka hazina wa kaunti kama faini ya kutolipa ushuru imesongeshwa kutoka Machi 31,2020 mpaka mwisho wa Mei 29, 2020, au (b) Amri 2020-4.
2. Nakala ya amri hii itapelekwa kwa Ofisi ya Utawala wa Mahakama ya Jimbo. Ofisi ya Utawala wa Mahakama ya Jimbo inatiwa moyo ihimize mahakimu wa mahakama ndogo kurekebisha amri kuhusu nyumba zilizofungwa kwa kukosa kutoa malipo iliyotolewa mwaka wa 2020 chini ya sehemu ndogo (5) ya sehemu 78k ya GPTA, MCL 211.78k(5), thabiti na kusongeshwa kwa tarehe ya mwisho chini ya sehemu ya 1.
3. Kama amri hii haikufutwa mapema, itaanza kufanya kazi punde tu itakapotolewa hadi mwisho wa (a) mei 29, 2020 au siku 30 baada ya kukomehswa kwa hali ya dharura chini ya sehemu ya 3 ya Amri ya Utendaji 2020-4.

Imetolewa chini ya mkono wangu na Nembo Kuu ya Jimbo la Michigan.

Tarehe: Machi 18, 2020

Saa: 3:39 Jioni



GRETCHEN WHITMER
GOVERNOR

Gavana:

WAZIRI WA SERIKALI YA JIMBO